

# Je! Uko Maafa Tayari?

**PANGA. ANDAA. KUISHI**



Australian Government



Queensland Government



TOWNSVILLE MULTICULTURAL SUPPORT GROUP INC.

**TMSG**



**TOWNSVILLE  
LOCAL DISASTER  
MANAGEMENT GROUP**





# Moto wa Kichaka

**Habari hii inahusu mambo ya kufanya kukiwa na moto wa kichaka.**

**Moto wa kichaka ni moto kubwa unaoweza:**

- kuenea haraka
- kutokea wakati wowote
- kuwa hatari.



Hatari inamaanisha kwamba unaweza kuumia. Kwa mfano, unaweza kuchomeka.



Ikiwa kuna onyo la moto wa kichaka ni lazima uamue kubaki au kuondoka.



Moto wa kichaka unaweza kukuumiza wewe na familia yako.

**PANGA. ANDAA. KUISHI**

## Je, moto wa kichaka unaweza kufanya nini?



Moto wa kichaka unaweza kuharibu nyumba yako.



Moto wa kichaka unaweza kuharibu vitu vilivyo nyumbani kwako, kwa mfano samani.

## Ili uwe tayari kwa moto wa kichaka unapaswa:



Kuwa na vifaa vya dharura.



Kupanga mambo ambayo wewe na familia yako mtafanya endapo kuna onyo la moto wa kichaka.



Pata bima kwa ajili ya nyumba yako na vifaa vilivyo ndani ya nyumba yako.



Unapaswa pia kusikiliza Redio na Runinga ya ABC kwa maonyo ya moto wa kichaka.



Kata nyasi ndefu na miti midogo iliyoko karibu na nyumba yako.

**Malipo ya bima ni pesa ambayo unaweza kupata kutoka kwenye kampuni ya bima jambo baya likitokea.**



# Tufani

**Habari hii inahusu mambo ya kufanya kukiwa na tufani.**

**Tufani ni hatari na inaweza kusababisha:**



Upepo mkali.



Ngurumo kubwa za radi.



Mafuriko.



Tufani inaweza kuwa hatari. Hatari inamaanisha kwamba unaweza kuumia. Ikiwa kuna onyo la tufani unapaswa kukaa ndani mpaka dhoruba iishe.

**PANGA. ANDAA. KUISHI**

## Je! Uko Maafa Tayari?

### Je, tufani inaweza kufanya nini?



Tufani inaweza kuharibu nyumba yako.



Tufani inaweza kuharibu vifaa vilivyo ndani ya nyumba yako, kwa mfano samani.



Tufani inaweza kukuumiza wewe na familia yako.

### Ili uwe tayari kwa tufani unapaswa:



Kuwa na vifaa vya dharura.



Kupanga mambo ambayo wewe na familia yako mtafanya endapo kuna onyo la tufani.



Pata bima kwa ajili ya nyumba yako na vifaa vilivyo ndani ya nyumba yako.



Unapaswa pia kusikiliza Redio na Runginga ya ABC kwa maonyo ya tufani.



Hakikisha kwamba nyumba na bustani yako iko salama.

**Malipo ya bima ni pesa ambayo unaweza kupata kutoka kwenye kampuni ya bima jambo baya likitokea.**





# Tetemko la ardhi

**Habari hii inahusu mambo ya kufanya kukiwa na tetemko la ardhi.**

**Tetemko la ardhi ni wakati ambapo ardhi inatetemeka.**



Matetemeko ya ardhi yanaweza kutokea wakati wowote, yanaweza kuwa makubwa au madogo, na ni hatari.



Hatari inamaanisha kwamba unaweza kuumia. Kwa mfano, kitu kinaweza kukuangukia.



Tetemeko la ardhi linaweza kukuumiza wewe na familia yako.

**PANGA. ANDAA. KUISHI**

## Je! Uko Maafa Tayari?

### Je, tetemeko la ardhi linaweza kufanya nini?



Tetemeko la ardhi linaweza kuharibu nyumba yako.



Tetemeko la ardhi linaweza kuharibu vitu vilivyo nyumbani kwako, kwa mfano samani.

### Ili uwe taayari kwa tetemeko la ardhi unapaswa:



Kuwa na vifaa vya dharura.



Kupanga mambo ambayo wewe na familia yako mtafanya endapo kuna onyo la tetemeko la ardhi.




Pata bima kwa ajili ya nyumba yako na vifaa vilivyo ndani ya nyumba yako.



Unapaswa pia kusikiliza Redio na Runginga ya ABC kwa maonyo ya tetemeko la ardhi.




Hakikisha kwamba vitu vilivyo nyumbani kwako havitakuangukia.




**Malipo ya bima ni pesa ambayo unaweza kupata kutoka kwenye kampuni ya bima jambo baya likitokea.**


### Wakati wa tetemeko la ardhi unapaswa:



**KUINAMA!**



**KUJIFUNIKA!**



**KUWA IMARA!**

**PANGA. ANDAA. KUISHI**





# Mafuriko

**Habari hii inahusu mambo ya kufanya kukiwa na mafuriko.**

**Mafuriko hutokea wakati ambapo maji yanafurika ardhi na kukuzuia kwenda nje.**



Mafuriko yanaweza kutokea wakati wowote, yanaweza kutokea polepole au haraka, na yanaweza kuwa hatari.



Hatari inamaanisha kwamba unaweza kuumia. Kwa mfano, unaweza kuanguka majini na kuzama.



Ikiwa kuna mafuriko usiendeshe gari kwenye maji.

**PANGA. ANDAA. KUISHI**

## Je! Uko Maafa Tayari?

### Je, mafuriko yanaweza kufanya nini?



Mafuriko yanaweza kukuumiza wewe na familia yako. Mafuriko yanaweza kuharibu nyumba yako.



Mafuriko yanaweza kuharibu vitu vilivyo nyumbani kwako, kwa mfano samani.

### Ili uwe tayari kwa mafuriko unapaswa:



Kuwa na vifaa vya dharura.



Kupanga mambo ambayo wewe na familia yako mtafanya endapo kuna onyo la mafuriko.



Pata bima kwa ajili ya nyumba yako na vifaa vilivyo ndani ya nyumba yako.



Hakikisha kwamba nyumba na bustani yako iko salama.



Weka vitu vilivyo nyumbani kwako juu.

**Malipo ya bima ni pesa ambayo unaweza kupata kutoka kwenye kampuni ya bima jambo baya likitokea.**



Unapaswa pia kusikiliza Redio na Runinga ya ABC kwa maonyo ya mafuriko

**PANGA. ANDAA. KUISHI**

# Hali mbaya ya Hewa

**Habari hii inahusu mambo ya kufanya kukiwa na hali mbaya ya hewa.**

**Hali mbaya ya hewa inaweza kuwa:**



Upepo mkali.



Ngurumo kubwa za radi.



Mvua kubwa ya mawe.



Hali mbaya ya hewa inaweza kutokea wakati wowote.



Hali mbaya ya hewa ni hatari. Hatari inamaanisha kwamba unaweza kuumia.



Hali mbaya ya hewa inaweza kukuumiza wewe na familia yako.

**PANGA. ANDAA. KUISHI**

## Je! Uko Maafa Tayari?

### Je, hali mbaya ya hewa inaweza kufanya nini?



Hali mbaya ya hewa inaweza kuharibu nyumba yako.



Hali mbaya ya hewa inaweza kuharibu vitu vilivyo nyumbani kwako, kwa mfano samani.

### Ili uwe tayari kwa hali mbaya ya hewa unapaswa:



Kuwa na vifaa vya dharura.



Kupanga mambo ambayo wewe na familia yako mtafanya endapo kuna onyo la hali mbaya ya hewa.



Pata bima kwa ajili ya nyumba yako na vifaa vilivyo ndani ya nyumba yako.



Unapaswa pia kusikiliza Redio na Ruinga ya ABC kwa maonyo ya hali mbaya ya hewa.



Hakikisha kwamba nyumba na bustani yako iko salama.

**Malipo ya bima ni pesa ambayo unaweza kupata kutoka kwenye kampuni ya bima jambo baya likitokea.**





# Joto Kali

**Habari hii inahusu mambo ya kufanya kukiwa na joto kali.**

**Joto kali ni:**

- Siku tatu au zaidi zenye hali ya hewa yenye joto jingi



Joto kali inaweza kutokea wakati wa miezi ya kiangazi – Desemba mpaka Februari



Joto kali inaweza kuwa hatari. Hatari inamaanisha kwamba unaweza kuumia.



Joto kali inaweza kukumiza wewe na familia yako.

---

**PANGA. ANDAA. KUISHI**

## Je! Uko Maafa Tayari?

### Je, joto kali inaweza kufanya nini?



Joto kali inaweza kuwaumiza watoto wachanga na wadogo.



Joto kali inaweza kuwaumiza wazee.



Joto kali inaweza kuwaumiza watu wenye hali za kimatibabu kama vile pumu.



Joto kali inaweza kuwaumiza watu wanaofanya kazi nje ya nyumba.



Joto kali inaweza kuwaumiza wanyama vipenzi.

### Ili uwe tayari kwa joto kali unapaswa:



Kunywa lita 2 hadi 3 za maji kila siku, hata kama hauna kiu.



Kupunguza unywaji wa pombe, vinywaji baridi, chai au kahawa.



Jaribu kula vyakula baridi, hasa saladi na tunda. Epuka kula vyakula vyenye protini nyingi ambavyo huongeza joto ya mwili na kuzidisha kupoteza ugiligili au maji.



Usiwaache watoto, watu wazima au wanyama kwenye magari yaliyoegeesha.




Epuka kwenda nje wakati ambapo kuna jua kali sana (saa 11 asubuhi-3 jioni).



Tumia feni au viyoyozi nyumbani ili kusikuwe na joto, au kaa sehemu nyingine kwenye kiyoyozi au mfumo wa kusafisha hewa.

**PANGA. ANDAA. KUISHI**





**Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti yetu: [disaster.townsville.qld.gov.au](https://disaster.townsville.qld.gov.au)**

Ingawa bidhaa hii imefadhiliwa na Serikali za Australia na Queensland,  
makala yaliyopo hapa hayawakilishi maoni ya Serikali yoyote kati ya hizo mbili.